# Utendakazi wa Hadithi za Watoto za Kiswahili katika Kubuni na Kupalilia Muonoulimwengu Wao

*Evans Mbuthia*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Makala haya nalenga kubainisha jinsi wahusika katika Hadithi za Watoto wanavyosawiriwa na waandishi tofauti. Hadithi za Watoto za Kiswahili zimeandikwa kwa wingi katika miaka ya hivi karibuni. Ni wazi kuwa mashirika mengi ya uchapishaji yameanza kukazia aina hii ya uandishi. Hii ni kutokana na imani kuwa hadithi hizi zina nafasi muhimu sana katika kuwasaidia wasomaji kufahamu mazingira yao na kujifahamu wao wenyewe. Hadithi za watoto pia zinaweza kuwasaidia katika kukuza uwezo wao wa kuelewa lugha na ulimwengu wao. Ni muhimu pia kutambua kuwa watoto hubuni ulimwengu wao kutokana na yale wanayosoma. Kutokana na msisimko huu wa kukazia aina hii ya uandishi baadhi ya vitabu vya Hadithi za Watoto vilivyoandikwa vimedhirisha mwegemeo usiofaa katika usawiri wa watoto wa jinsia tofauti bila kuwazia athari ya mtindo huo wa uandishi. Kwa hiyo, makala haya yanatathmini namna wahusika wa jinsia mbali mbali walivyokuzwa na baadhi ya waandishi na athari za uteuzi wao. Ni bayana kwamba waandishi wengi wamewasawiri wahusika wa jinsia tofauti kwa usawa lakini ni kweli pia baadhi ya waandishi wamewasawiri wahusika wavulana kwa njia hasi na wasichana kwa njia chanya na kinyume chake pia. Vilevile majukumu yao yametofautishwa kwa njia ambayo hailandani na ukweli wa mambo katika ulimwengu wa sasa. Mjadala wa makala haya utajikita katika vitabu tofauti vya hadithi za watoto.**

**Maneno Muhimu:** *Mtazamo Ulimwengu, Sosholojia ya Kifasihi*

**Utangulizi**

Fasihi ina majukumu mengi sana. Mojawapo ni kumshirikisha mtu binafsi katika mambo tofauti tofauti ya kijamii. Jukumu hili hutekelezwa na tanzu zote za fasihi kupitia vipera vyake mbalimbali. Kazi yoyote ya kifasihi huwa inalenga hadhira fulani. Ukweli huu ndiyo unaoifanya fasihi ya watoto kuwa fani maalum ya fasihi inayowalenga watoto. Kwa mujibu wa Matundura (2007), fasihi ya watoto hutambulishwa na sifa kadhaa kama vile:

> Huandikwa (hasa na watu wazima) kwa lengo la kusomwa na hadhira ya watoto, Huwa na wahusika ambao aghalabu wengi huwa ni watoto.

Hata hivyo baadhi ya vitabu vya fasihi ya watoto huwa na wahusika ambao ni watu wazima, wanyama, mazimwi na kadhalika. Sifa nyingine mahsusi za hadithi za watoto ni kama vile :

i. Hadithi huwa fupi na sahili
ii. Huandikwa kwa lugha na msuko sahili
iii. Hujaribu kuwaelimisha watoto kuhusu masuala ya jamii, mienendo yao mbali mbali na kuwa na Hadithi za Fantasia na Usimulizi wa Ugunduzi wa Mambo Mapya.
iv. Mara nyingi hadithi huishia kwa furaha huku wema ukishamiri dhidi ya uovu. Aidha, fasihi ya watoto huandikwa kwa lengo la kutoa funzo fulani.

Maelezo hayo yanaakisi hali halisi katika hadithi fupi za watoto. Aghalabu watoto hubuni ulimwengu wao kutokana na mambo wanayoyaona au wanayoyasoma kutoka katika vitabu vya fasihi.

Waandishi mbalimbali wa hadithi za watoto wamebuni taswira tofauti kuhusu ulimwengu unaowazingira watoto. Je katika uandishi wa hadithi za watoto kuna taswira inayofaa au isiyofaa? Swali hili litajibiwa katika makali hii kwa kuchunguza muonoulimwengu ambao unaangaziwa katika vitabu vitakavyoteuliwa.

Hadhira hii huweza kubuni mtazamo ulimwengu ambao kwa kiasi fulani umeimarishwa na kazi za kifasihi wanazozisoma. Muonoulimwengu ni jinsi jamii inavyotagusana na mambo mbali mbali.

Muonoulimwengu unahusu mahusiano ya wanajamii na wenzao, na hata na wageni. Unahusu utamaduni na imani za jamii na namna ambavyo wanajamii hukabiliana na changamoto zinazowakabili ziwe za kitamaduni, kisiasa au kiuchumi.

Ni bayana kwamba muonoulimwengu wa jamii fulani hukuzwa na kupaliliwa kupitia maingiliano ya kijamii. Kwa hivyo ni wazi kuwa watoto na vijana huelewa muonoulimwengu wa jamii yao kutokana na mwingiliano na wazazi na wanajamii kwa jumla.

Siku hizi kwa sababu ya vyombo vya habari na vitabu, muonoulimwengu huweza kupanuka na kubadilika. Watoto wadogo ambao bado wako shuleni hukumbana na habari nyingi kutoka kwenye vitabu vya Hadithi ambavyo pia huwa na mchango muhimu kuhusu mtazamo wao wa ulimwengu. kwa kutegemea mitindo na mitazamo ya waandishi, watoto wanaweza kufaidi au kutofaidi kutokana na taswira watakazokumbana nazo katika vitabu mbalimbali.

Kwa kuwa hadhira huwa imegawanyika kijinsia, makala haya yanahoji namna ambavyo kila jinsia ya wasomaji invyoathirika kutokana na usomaji wa vitabu vilivyoteuliwa. Makala haya yanajadili kama mtazamo ulimwengu wa wasomaji utakuwa chanya au hasi kwa kutegemea namna hadithi anuwai zilivyowasilishwa kwa hadhira.

Vitabu vya hadithi vya watoto vilioandikwa kwa Kiswahili ni vingi mno. Mwandishi amefanya uteuzi wa makusudi wa vitabu mahsusi ambavyo vitachangia mjadala wake. Vitabu viitakavyosawiriwa katika makala haya ni vifuatavyo:

i. *Mwanasayansi cha* Kabaji, E. (2013)
ii. *Ndoto ya Riziki* cha Kimutai, R. (2003)
iii. *Ndoto ya Mwanafunzi cha* Manji, A. (2013)
iv. *Sungura na Binti Mfalme cha* Mpesha, N. (2007)
v. *Nipe Sababu* cha Musembi, N. (2009)
vi. *Ngamia Mpole* cha Nandwa, R. (2015)

**Udurusu wa Yalioandikwa**

Fasihi ya watoto imetafitiwa na wasomi mbalimbali. Nchini Kenya utafiti huu hasa umekuwa ukiendelezwa na wanafunzi wa vyuo vikuu hasa wanapoandika tasnifu zao. Baadhi ya walioandika tasnifu zao kuhusu Fasihi ya Watoto ni pamoja na: Ngugi (1997), Mpesha (1996), Matundura (2007) na Ngugi (2009).

Utafiti wa Mpesha (1996) ulihusu fasihi ya watoto nchini Tanzania. Mpesha alichunguza ukuaji na maendeleo ya Fasihi ya Watoto nchini Tanzania kwa kurejelea vitabu vya hadithi za watoto vilivyoandikwa kwa Kiswahili kutoka nchini Tanzania. Katika utafiti wake, Mpesha (khj) alitambua dhima ya fasihi ya watoto katika jamii. Utafiti wa Mpesha uliufaa huu wetu kwa vile ulithibitisha kuwa vitabu vya hadithi za watoto huakisi hali halisi ya jamii na vile vile hadithi za watoto huwa si ngano tu zenye umapokeo wa daima, bali ni usawiri wa jamii. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na wetu kwa kuwa wake ulihusu ukuaji na maendeleo ya Fasihi ya Watoto ilhali wetu unahusu athari ya usawiri wa watoto katika hadithi teule za watoto.

Karuga (2005) alihakiki vitabu teule vya hadithi vinavyosomwa katika shule za msingi nchini Kenya kwa kuchunguza fani na maudhui. Alieleza umuhimu wa fani katika kumwezesha mwandishi huwasilisha mawazo yake kwa hadhira. Utafiti wake ni muhimu kwetu kwa kuwa ulieleza wahusika kuwa mojawapo wa sifa kuu za vitabu vya hadithi za watoto. Utafiti huo ulitupatia msukumo wa kuchunguza usawiri wa wahusika watoto. Utafiti wa Karuga ni tofauti na wetu kwa vile yeye alichunguza fani na maudhui ilhali sisi tunajikita katika athari ya njia tofauti za usawiri wa wahusika watoto.

Mwanzi (2006) katika makala yake "Children's Literature: the concept of socializing the young'' (Fasihi ya Watoto: dhana ya kuwashirikisha watoto katika mambo ya kijamii) anachukulia kuwa haja ya kutekeleza jukumu lilotajwa hujitokeza katika Fasihi ya Watoto ulimwenguni kote. Anaongezea kuwa ilhamu ya kutekeleza jukumu hili ndiyo msukumo mkubwa sana katika uandishi wa Fasihi ya watoto.

Matundura (2007) alitafiti kuhusu taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Matundura alilenga kuchunguza namna ambavyo waandishi wanavyoweza kubuni taswira bunifu zinazolenga maswala ya kijinsia katika kazi zao. Alikuwa na msimamo ya kwamba waandishi wanaweza kusababisha hali zisizopendeza katika kazi zao kwa kuonyesha jinsia moja kwa njia isiyofaa.

Miricho (2014) alichunguza namna watoto wa kiume wanavyopuuzwa katika familia katika hadithi alizozichunguza. Alichukua msimamo ya kuwa jambo hili huenda likawafanya kutojiamini kama wenzao wa kike na kuishia kuwa watu wasiotimiza malengo mema maishani.

Kazi tulizozipitia zinachangia makala haya kwa njia mbili muhimu. Mosi zinaonyesha kuwa lengo muhimu linalochochea uandishi wa Fasihi ya Watoto; ni kuwashirikisha katika asasi tofauti za kijamii na pili zinaonyesha athari hasi inayosababishwa na kutochukua tahadhari muhimu katika malezi ya watoto.

**Msingi wa Kinadharia**

Nadharia ya Soshiolojia ya Kifasihi hutumika katika kuchanganua masuala ya kijamii. Wellek na Warren (1978: 23) wanaeleza kwamba, "Fasihi huibuka kutokana na taasisi mbalimbali za kijamii na katika jamii za kiasili mpaka baina ya ushairi, itikadi, michezo na kazi ulikuwa mwembamba sana'' (uk23). Wanaongeza kwamba "maswala mengi ambayo huibuka kutoka kwenye kazi za kifasihi huwa ya kijamii, kwa mfano kuhusu utamaduni, kaida, ishara na visa asili''.

Hadithi nyingi za watoto zinaafiki ukweli huu. Kuna zile ambazo zinagusia mambo haya kijuujuu na kuna zile ambazo zinayazamia. Kwa jumla, hadithi hizo huwa na athari kwa watoto.

Ni dhahiri kwamba binadamu anaishi katika jamii na wala sio kwenye ombwe tupu. Hivyo, kila tajriba anayoipitia sharti ichunguzwe katika mkabala wa jamii yake. Kulingana na Witte (1978: 8). jamii ni "kama kalibu inayompatia mwanadamu umbo Fulani". Warren (1978: 215) anakubaliana na wazo hili anapoeleza kuwa:

> Mtazamo wa kisholojia...Utasaidia kuonyesha jinsi tajriba za mwanadamu ambazo ingawaje zinaweza kuwa zimefungwa na wakati na maeneo zinavyoweza kufanywa za kudumu katika Fasihi.

Maelezo hayo yanadhihirisha kuwa hadithi za watoto pamoja na kuwatumbuiza huwa na athari kubwa katika maisha yao na jinsi wanavyyouona ulimwengu. Hii ina maana kuwa hadhira ya hadithi hizi huweza kujinasibisha na mienendo na tajriba za wahusika katika hadithi wanazosoma.

Nebbia (2016: 16) anaeleza:

> Ubaguzi wa kijinsia katika fasihi husababisha ujitambuzi na maendeleo ya kitabia miongoni mwa Watoto…ubaguzi wa kijinsia hupaliliwa na jamii na kupokezwa watoto wakiwa wachanga. Watoto huishia kumiliki Imani hizi kutokana vielelezo vibaya kwenye Fasihi ya Watoto.

Kazi zinazochunguzwa katika makala haya zina mifano ya wahusika vielezo waliosawiriwa kwa njia tofauti.

**Matokeo na Mjadala**

Katika sehemu hii kauli za kijumla kuhusu hadithi zimetolewa ili kuupa mjadala muelekeo. Aidha, kila hadithi imerejelewa kimuhtasari na tathmini kuhusu muonoulimwengu wa wahusika imetolewa.

**Maelezo ya Jumla Kuhusu Hadithi Zilizoteuliwa**

Vitabu vilivyoteuliwa vimegawanyika katika makundi manne mahsusi. Kwanza kuna kimoja ambacho kinazungumzia watoto wa jinsia zote mbili kwa njia horomo bila muegemeo wa kiupendeleo (*Ngamia Mpole* cha Nandwa). Pili ni vitabu ambavyo vinasawiri jinsia ya kike kwa njia hasi ingawaje si kwa mtindo wa moja kwa moja (*Sungura na Binti Mfalme* cha Mpesha na *Mwanasayansi* cha Kabaji). Tatu ni vitabu vinavyosawiri kila mojawapo ya jinsia kwa njia chanya (*Hongera Mwanangu* cha Obura na *Ndoto ya Riziki* cha Kimutai) Kundi la mwisho linasawiri jinsia moja kwa njia hasi(*Ndoto ya mwanafunzi* cha Manji na *Nipe sababu* cha Musembi).

**Muhtasari na Tathmini ya *Ngamia Mpole***
Hadithi hii inahusu watoto wawili wadogo; mmoja wa darasa la kwanza na mwingine wa chekechea pamoja na wazazi wao. Bonga Maarufu alikuwa darasa la kwanza na dadake alikuwa chekechea. Baba yao anaitwa Daudi Maarufu ambaye ni Daktari wa meno, na mama yao Lena Maarufu ni fundi wa nguo.

Katika hadithi hii watoto wanapelekwa matembezini na baba yao. Huko matembezini wanajifurahisha kwa kuchorwa uso na kwa kumpanda ngamia. Mwendeshaji ngamia anawasimulia kuhusu ngamia wake. Vilevile anawaeleza kuhusu watu wengine ambao huwatesa wanyama tabia ambayo haifai kamwe.

Baada ya ziara, watoto wanarudi nyumbani wamefurahi sana. Furaha yao inatokana na kutembezwa na kufurahia kumpanda ngamia tukio ambalo ni la kipekee sana kwao. Wanashanga kwa nini babu yao hana ngamia. Wanaelezwa kuwa ngamia hupatikana katika maeneo kame ya nchi.

Hadithi hii inawasawiri watoto hawa kwa njia horomo. Hakuna mapendeleo ya kijinsia. Bonga na dada yake wote wamesawiriwa kwa njia sawa. Hakuna yeyote anayeonekana mwerevu kumzidi mwenzake. Hakuna aliyesawiriwa kama mjinga. Wote wawili wameonyeshwa kama watoto watiifu ambao wanawasikiliza wazazi wao bila ya kushiriki katika mambo yasiyofaa.

**Muhtasari na Tathmini ya *Sungura na Binti Mfalme* na *Mwanasayansi***
Katika Sungura na Binti Mfalme ya Mpesha tunahadithiwa kumhusu Binti wa mfalme aliyekuwa msichana mrembo sana. Mwandishi anaeleza kuwa binti huyu alikuwa daima akitabasamu. Uzuri huu wa kimaumbile ndio uliokuwa kivutio kwa wanaume wengi ambao walitaka kumuoa.

Urembo wake uliwavutia watu wengi na wa namna mbalimbali. Watu hawa walikuwa wametoka sehemu mbali mbali za nchi. Jambo hili lilimtia wasiwasi na hata wazazi wake pia waliingiwa na hofu. Hali hii ilimpelekea baba yake kutoa agizo kuwa atakayemuoa bintiye ni yule atakayeweza kunywa maji yaliyochemshwa.

Mwandishi hajamtunukia sifa nyingine inayopendeza ila uzuri wake wa sura. Uzuri huu unawafanya watu maarufu na maumbile tofauti kufanya juhudi za kumuoa. Wote wanashindwa ila sungura mjanja anayefaulu kupita mtihani wa kunywa maji yaliyokuwa ya moto kiasi cha kuchemka. Ujumbe unaootokana na hadithi hii unahusu jinsia ya kike kutamanika tu kwa sababu ya urembo. Bila ya urembo binti mfalme hangekuwa na sifa nyingine ambayo ingewavutia watu wengi ambao walikuwa na hamu kubwa ya kumuoa.

*Mwanasayansi* ni hadithi ambayo ina wahusika wawili wakuu Tami na babake. Tami alikuwa kijana mdogo wa shule ambaye alikuwa na hamu kubwa ya kuwa mwanasayansi. Kutokana na azma hii ambayo alikuwa nayo tangu awe mtoto mdogo alipenda kusoma kila alipopata wakati. Alikuwa na wazo la kuwafuga ndege. Baba yake alimshauri kuwa ingefaa asome kuhusu jambo hili na pia kuwauliza wanaofahamu ili waweze kumshauri.

Baada ya kumrai baba yake kwa muda mrefu,baba yake alimpeleka maktabani. Mkutubi alimuonyesha vitabu kadhaa kuhusu ndege na hatimaye Tami aliomba kitabu kimoja. Tami alikisoma kitabu hicho kwa bidii na kuishia kujua mengi kuhusu aina tofauti za ndege. Alijiona tayari anaweza kufuga ndege kwa hivyo akawaomba wazazi wake waanze kufuga ndege.

Katika mwanasayansi hatukutani na mwanafunzi wa jinsia ya kike ambaye anavutiwa na sayansi au hataa sanaa. Tangu mwanzo hadi mwisho mwanafunzi ni wa jinsia moja tu. Mama yake Tami hatokezi katika kisa hiki. Ni bibi yake tu anayetokeza wakati anamuinga mwewe aliyekuwa amekivamia kifaranga chake.

Kisa hiki cha kusisimua kinamulika mhusika wa jinsia ya kiume ambaye anapendelea sayansi. Pia ni baba ambaye anampatia moyo kuhusu somo hili. Msomaji wa jinsia ya kike anaweza kupatwa na wazo kuwa taaluma ya sayansi inafunganamishwa na jinsia ya kiume. Kwa hivyo kisa hiki bila makusudio ya mwandishi kinaendeleza ile kasumba miongoni mwa baadhi ya wazazi na wanafunzi kuwa masomo ya kisayansi na kiteknolojia ni ya jinsia ya kiume.

Swala hili limechangiwa na wataalamu wengi na hata mashirika kama vile UNESCO. Katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake ya mwaka wa 2022, UNESCO na mashirika mengine ya kitaifa

yanayoshughulikia maswala ya masomo walikuwa na konganao ambapo walihimiza wanafunzi, wazazi, na serikali kushirikiana katika kuangamiza kasumba za kijinsia katika masomo. Swala hili pia limejadiliwa na Jacobs (2016) aliyeeleza kuwa waktubi wahakikishe kwamba vitabu wanavyopendekeza visiwe vile vinavyosawiri njia wahusika wa jinsia yoyote kwa njia hasi kama kielelezo kwa jinsia husika.

**Muhtasari na Tathmini ya *Hongera Mwanangu* na *Ndoto ya Riziki***

Katika *Hongera Mwanagu* ya Kabaji mwandishi anatusimulia kuhusu kisa cha jamii ya Maizi ambayo ilikuwa inatatizwa na kero ya wizi. Maizi alikuwa mkulima na alitegemea kupata pato kutokana na maziwa kutoka kwa ngombe wake. Aligundua kuwa kuna mwizi ambaye alikuwa akiwakama ngombe wake kwa siri na kutoweka na maziwa.

Mafamba ambaye alikuwa mfanyakazi wao pale shambani ndiye aliyekuwa akitekeleza wizi huu. Alikuwa akiingia zizini usiku na kufanya uovu wake gizani. Waajiri wake hawakumshuku. Tatizo hili liliwakera sana. Mtoto wao Bamba aliamua kutegea kitandiwili hiki. Wazazi wake walikuwa hawaamini kuwa anaweza kutatua shida ambayo hata baba yake hakuelewa namna ya kukabiliana nayo. Hata hivyo walimpatia nafasi ya kujaribu kumkamata mwizi.

Juhudi zake za kushika doria huku akiandamana na mbwa wake watatu hazikufua dafu. Kwa hivyo aliamua kubadilisha mbinu. Alikwenda zizini usiku kisiri na kumwondoa ngombe wa maziwa na kumfunga punda zizini. Bamba hakumhusisha yeyote katika shughuli hii, Mafamba hakufahamu kuhusu mtego aliowekewa. Kama kawaida aliingia zizini na zana yake muhimu - Ndoo ya kubebea maziwa. Alinyata hadi punda alipokuwepo huku akidhania ni ngombe aliyezoea kumkama. Hakuweza kuona vizuri kwa sababu ilikuwa usiku. Mara tu alipojaribu kutafuta titi lake alipigwa mateke dhoruba moja! Aliwika kwa uchungu na kuzirai. Kulipokucha alikutwa hapo amelala na kuchukuliwa kwa machela hadi hospitali.

Katika Hadithi hii tatizo lintatuliwa na kijana mwanaume ambaye anatumia busara yake. Kisa hiki hakielekei kutweza jinsia yoyote kwa sababu mkazo ni uwezo wa kijana ambaye yuko na umri mdogo wa kuitatulia jamii yake shida ambayo ilikuwa kero kubwa kwao.

*Ndoto ya Riziki* ni Hadithi inayodhibitisha kuwa penye nia pana njia. Mhusika mkuu Riziki licha ya kuwa alikuwa msichana alifanya juhudi za kuwadhibitishia rika zake kuwa aliweza kufanya mambo ambayo waliweza kuyafanya hata kama alikuwa msichana.

Alikuwa na azimio la kuwa daktari. Ingawaje mara nyingi hakuhudhuria masomo kwa sababu ya ukosefu wa karo alijikaza na kuibuka kuwa mwanafunzi hodari. Alikuwa mtiifu kwa wazazi wake na kwa hivyo aliweza kutekeleza majukumu yake ya nyumbani na ya shuleni. Alipofika Chuo kikuu hakukubali himizo na msukumo wa marafiki zake za kuingilia mambo ya anasa. Msimamo wake kuhusu azimio la kujiendeleza kimasomo na kuwa daktari haukutikiswa na uhuru mkubwa waliokuwa nao katika chuo kikuu.

Hadithi hii inaibua maswala kadhaa. Katika utoto wake rafiki mkubwa wa Riziki alikuwa Hannah ambaye alitoka katika familia iliyokuwa imeimarika kiuchumi. Licha ya tofauti hizi za kiuchumi walidumisha urafiki wao.jambo la pili ni kuwa Riziki alikuwa na azimio la kuwa daktari ingawa alitoka katika jamii ambayo haikuwa na nguvu za kiuchumi.

Kwa hivyo, kisa hiki kinampa msomaji mafunzo kemkem. Inabainika kuwa urafiki haustahili kutegemezwa tabaka na pili hata watoto wa kike wanaweza kufanikiwa katika taaluma ambazo kasumba za kijamii zinachukulia kuwa zinastahili kuwa za watoto wa kiume.

**Muhtasari na tathmini ya *Nipe Sababu* na *Ndoto ya Mwanafunzi***

Hadithi hizi mbili zinaingia katika mkumbo mmoja kwa sababu ni hadithi ambazo zinatoa funzo kwa kuonyesha jinsi uvunjaji sheria unvyoweza kumtia mtu mashakani. Katika kila mojawapo vijana wavulana wanakaidi sheria, na hatima ya vitendo vyao inakuwa mbaya.

Katika *Nipe Sababu* ya Nandwa watoto watatu wa shule ya msingi; Katu, Safari na Chalii wanatumia mapumziko yao ya shule katika shughuli za uwindaji. Wanawawinda wanyama wadogo kama vile sungura na swara.

Utundu wao pia unawapelekea kumfukuza nyani ambaye alikuwa na mtoto wake. Nyani analazimika kutoweka porini. Hatimaye wanauona mzinga wa nyuki. Licha ya kuonywa na wenzake kuhusu hatari ya nyuki Katu anashikilia kuwa atawelenga kwa manati yake ili wafurahie asali. Katu anaulenga mzinga. Nyuki wanawashambulia kwa hasara. Kila mmoja wao anatawanyika na mayowe yanatanda hewani. Baadaye Katu anashambuliwa hadi anavua shati ili kujaribu kuwafukuza nyuki. Anaanguka chini na kuzirai. Baba yake anapotokea anamkuta Chalii amelala kifudifudi. Juhudi zake za kumuasha hazifai kitu. Anambeba na kumpeleka nyumbani. Baada ya kupata afueni siku tatu baadaye anaonywa dhidi ya uharibifu wa mizinga ya nyuki kwa sababu nyuki ndiyo kitega uchumi katika eneo hilo. Baba yake anapotaka kumuadhibu anaomba ahurumiwe kwa sababu tayari nyuki walikuwa wamempatia adhaabu ya kutosha.

Katika *Ndoto ya Mwanafunzi* ya Manji vijana wawili wanaamua kuzamia meli. Juma na rafikiye Hamisi ambao walikuwa wakiishi karibu na bahari walikuwa wamesikia visa vya vijana waliozamia meli na hatimaye kufanikiwa kimaisha katika mataifa ya nje. Walianza kukuza wazo hili kutokana na kutangamana na vijana wazembe ambao walipitisha muda mwingi wakiwa wamebarizi majiani. Vijana hawa walikuwa wameacha shule na kuingilia wizi na utumiaji wa dawa za kulevya.

Siku waliyopanga ya kufanya uhalifu wao ilipofika walijiandaa kwa kununua maji na biskuti za kula wakiwa safarini. Waliingia kisiri katika meli ambayo ilikuwa inaelekea ulaya na kujificha kwenye chumba cha injini amabako si rahisi kugunduliwa. Humo walipata dhiki na maaisha yao kuwa hatarini kutokana na moshi uliotoka kwenye injini.

Hatimaye meli ilifika katika pwani fulani. Walifikiri wamefika ulaya kumbe walikuwa Mauritius. Walitoka kwenye meli na kuingia majini kwa nia ya kuogelea hadi pwani. Arobaini yao ilikuwa imefika kwa sababu walikamatwa na askari wa kushika doria pwani. Walipelekwa hospitali na baadaye kufungwa jela. Hatimaye walihamishiwa katika jela ya kwao. Kwa hiyo juhudi zao za kukimbilia nchi nyingine kinyume cha sheria haikuwafaa na badala yake waliishia kufungwa jela.

Hadithi hii inadhihirisha hatari ya fikira potovu miongoni mwa vijana ya kuwa hawawezi kujiendeleza nchini mwao lakini ng'ambo ndiko kwenye natija ya kufurahiwa. Vilevile ni hadithi yenye onyo kuhusu vijana wa shule kutangamana na wale ambao wamekaidi sheria za wazazi na kutumia muda wao mabarabarani kwa nia ya kuiba au kushiriki uvunjaji sheria wa aina mbali mbali.

Katika hadithi hii ni bayana ya kwamba ni vijana wa kiume ndiyo wanachukua hatua hizi za kipotovu. Hadithi hii haina wahusika wa kike. Ni kama kwamba wandishi wanadokeza kuwa tabia ya aina hii isiyofaa aghalabu huendelezwa na vijana wa kiume.

**Hitimisho**

Swala la muonoulimwengu linatagusana na fasihi kwa sababu fasihi hufunua ulimwengu na kuijulisha hadhira kuhusu mambo mengi. Hadithi za watoto hutekeleza jukumu hili kwa njia maalum. Hii ni kwa sababu watoto huwa katika hali ya kukua na kufanya majaribio ya mambo mbalimbali. Kulingana na Mwanzi (2006), Hadithi za Mashujaa waliopambana na mazimwi ni kielelezo cha jinsi Fasihi au hadithi za watoto zinaweza kutumika katika kusisitiza maswala ya haki katika jamii.

Katika nyingi za hadithi hizi watoto watundu hujipata mashakani wanapokabiliwa na zimwi lakini wao huokolewa na mashujaa wa jamii. Ikumbukwe kwamba jamii ni kama kalibu ambamo wanajamii wakipitishwa pale aghalabu huweza kuchukua umbo jipya linalolandana na tajiriba hizo mpya. Ni wazi kuwa ni rahisi kwa watu wazima kujiepusha na athari mbaya kuwaliko watoto ambao aghalabu huwa katika kipindi cha majaribio bila ya kuwazia hatima ya vitendo vyao. Pia kuna watu wengine wazima ambao hushindwa kujinasua kutokana na mitego ya msukumo wa kirika na kuishia kuathiriwa pabaya au wao wenyewe maksudi kujiamulia mtindo mbovu wa maisha. Hatima ya uteuzi wao mbaya huwaletea mashaka baadaye.

Ni wazi kuwa katika mtagusano na hadithi zilizoteuliwa katika mjadala huu hadhira inafunguliwa mtazamo ulimwengu. Mtazamo ulimwengu wanaofunguliwa unaweza kuwa kwa neema au kwa shari.unaweza kuwa wa kujenga au kubomoa wahusika katika hadithi zinazohusika.

Katika *Ngamia Mpole* mwandishi anawafungulia wanafunzi ulimwengu wa haki dhidi ya wanyama.mwendesha ngamia Ali Dabo aliwaeleza kuwa si haki kuwatesa wanyama. Aliwasimulia

kisa cha mtu mmoja aliyewatesa punda na ngamia wake. Kutokana na dhuluma hii madaktari wa wanyama walilazimika kuwatibu wanyama hao na maofisa wanaoshughulikia haki za wanyama kumlazimisha kulipia gharama ya matibabu.

Katika Hadithi ya *Sungura na Binti Mfalme* msisitizo kuhusu mhusika mkuu ni urembo wa mhusika mkuu. Mwandishi hatuelezi kuhusu silika ya mhusika huyu. Urembo wake ndiyo kivutio chake kikuu. Kutokana na hadithi hii kuna uwezekano kwa wasomaji kuwa na mtazamo kuwa urembo ndiyo kipawa chenye uzito kwa wasichana.

Katika *Mwanasayansi* Tami kijana wa kiume anapendelea sayansi. Anamrai baba yake kumsaidia kuhusu mambo ya kisayansi. Hakuna mhusika wa jinsia nyingine ambaye anatokeza kwenye kisa hiki. Kisa hiki kinakoleza kasumba ya imani kuwa sayansi ni somo gumu ambalo linaweza kudhibitiwa na watoto wa kiume tu. Ni kama kwamba kuna uchukulizi ya kuwa watoto wa jinsia ya kike wajishughulishe na masomo ya kisanaa.

*Ndoto ya Riziki* na *Hongera Mwanangu* ni hadithi mbili ambazo mtazamo ulimwengu chanya. Katika *Ndoto ya Riziki* kuna mhusika msichana ambaye anajiamini na hata unyonge wa familia yao wa kiuchumi haumvunji moyo. Anakazania taaluma ya udakitari na ndoto yake inatimia. Pia mhusika mwingine wa jinsia ya kike Bi, Mateo ni daktari na anamhimiza kujikaza katika masomo ya kisayansi ili atimize ndoto yake.

Katika *Hongera Mwanangu* Bamba ambaye alikuwa kijana wa miaka kumi na miwili alijidhihirisha kuwa jasiri na kufanya mipango ya kumkamata mwizi ambaye alikuwa anaitatiza jamii yake. Hadithi hii kwa hakika inafungua macho vijana wasikubali kupuuzwa kwa sababu ya umri wao mdogo kwa sababu licha ya hali hiyo wanaweza kuifaidisha jamii kama alivyofanya Bonga. Hadithi hii vilevile inaupanua mtazamo ulimwengu wa wazee dhidi ya vijana inadhihirisha kuwa pia vijana wanaweza kutegemewa.

Kwa hivyo ni dhari kuwa kupitia hadithi za watoto vipengele anuwai vya muonoulimwengu huweza kujadiliwa. Vipengele hivi ni kama vile; majukumu ya kijamii, elimu na uteuzi wa taaluma na silika njema. Waandishi katika hadithi zilizoteuliwa wamewasilisha mada zao kwa kuonyesha namna muonoulimwengu unavyoweza kudhihirishiwa hadhira kwa nia ya kuwasaidia waige mambo yanayofaa na wajitenge na yale yasiyofaa. Waandishi wamefaulu katika kazi zao lakini ili kuhakikisha wasomaji wanakuwa na mtagusano razini na hadithi za watoto basi ni muhimu kwa wao kusoma hadithi nyingi zenye misimamo tofauti ili wawe na mawazo sahihi juu ya jinsia tofauti.

**Marejeleo**


Eagleton, T. (1996). *Literary Theory*. London: Blackwell Publishing.

Escarpit, R. (1966). *Sociology of Literature*. London: Frank and Cass.

Glicksberg, C. L. (1987). *Literature and Society: The Sociology of Literature.* (Wh.). Dandson P. Cambrige: Chadwik Harley.

Grenby, M. O. (2008). *Children's Literature*. Edinburg: Edinburg University Press.

Hunt, P. (Mh.). (1994). *An Introduction to Children Literature*. New York: Oxford University Press.

Jacob, K. (2018). *Gender Issues in Young Adults Literature*. Indiana: Indiana University Press.

Kabaji, E. (2013). *Mwanasayansi.* Nairobi: Oxford University Press.

Kimutai, R. (2003). *Ndoto ya Riziki*. Nairobi: Oxford University Press.

Laurenson, D. T. na Swingewood, A. (1972). *The Sociology of Literature*. London: Macgibbon Ltd.

Manji, A. (2013). *Ndoto ya Mwanafunzi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Matundura, B. (2005). *Mwepesi wa Kusahau*. Nairobi: Phoenix.

Matundura, B. (2007). *Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi

Matundura, B. (2014). *Likizo ya Mkosi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbatiah, A. M. (1999). *The Origin and Development of Swahili Thesis Novel in Tanzania.* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbuthia, E. M. (2005). *A Thematic and Stylistic Analysis of Kiswahili Short Stories.* Tasnifu ya Uzamifu chuo kikuu cha Nairobi

Mpesha, N. (2007). *Sungura na Binti Mfalme.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Musembi, N. (2009). *Nipe Sababu*. Nairobi: Oxford University Press.

Nandwa, R. (2015). *Ngamia Mpole*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Nebbia, C. C. (2016). *Gender Stereotypes in Children's Literature*. MA Thesis, University of Northern Iowa.

Ngugi, P. M. (2009). *The State of Children Literature in Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu Cha Vienna, Austria.

Ngugi, P. M. (2014). Miaka Hamsini ya Fasihi ya Watoto Katika Kiswahili Nchini Kenya. Katika Simala, I. et al. (wh) Twaweza Communications, Nairobi

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Odaga, A. B. (1985). *Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau

Thiong'o, N. (1978). Literature in Society. In Gachukia, E. na Akivaga, S. K. (Wh.), *Teaching of African Literature in Schools.* KLB.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Warren, A. na Wellek, R. (1973). *Theory of Literature.* London: Penguin Books.